

Pambazuko

Toleo Namba 067

Jumatatu Machi 25-31, 2024

Lulandala hebu acha
'urongo' bhana!

UK. 5



Jicho la Tai



**Biashara ya hewa
ukaa, mkondo
mwingine wa
ukoloni mamboleo**

UK. 12-13

**Aliyefungwa
miaka 23
kwa ujangili
atoroka**

**Tanapa
yaja
kivingine**

UK. 8

UK. 6



JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye
namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Tahariri

Tuanzishe kurugenzi huru kuchunguza Polisi

SIFA za Jeshi la Polisi Tanzania zimekuwa zikibadilikabadilika kila mara kutegemea nani ni mkuu wa nchi na zaidi sana nani ni Inspekta Generali (IGP) kwa wakati huo.

Hakuna siri hata kidogo kwamba kila IGP anakuwa na zama zake; wapo waliofanya kazi vizuri – bila kujiingiza kwenye mtungo wa majambazi, wauza dawa za kulevyu, majangili na hata wanyang'anyi wengine, wakiwamo mafisadi.

Lakini pia wapo wakuu wa jeshi letu la Polisi walioamua kujiunga na magenge ya hovyoy kwa ajili ya kupata utajiri haramu wa harakaharaka.

Hawa wakuu wa kundi la pili ndio walioharibu kabisa nidhamu na sifa ya jeshi hilo lenye majukumu makubwa ya kulinda watu na mali zao. Hawa walishiriki kutesa, kubambika kesi na kuamuru wasaidizi wao kupora mali halali za wananchi ilimradi wao wapate kikubwa na neema kwa kuumiza wengine.

Ni hawa wa kundi la pili ndiyo walikuwa wakijiona mungu-watu, kiasi kwamba hawakuwa hata na chembe ya kumuogopa Amiri Jeshi Mkuu kwa sababu ambazo wanazijua wao wenyewe.

Hivi karibuni kumekuwa na taarifa kwamba watuhumiwa wamepokwa mali zao, kuteswa na hata baadhi ya watuhumiwa kufia mikononi mwa watendaji wa jeshi hilo.

Kunapotokea matukio haya ya hovyoy, ni watendaji wa jeshi hilihilo ndiyo hupangwa kuchunguza kilichotokea, hatua ambayo, kwa mizania yoyote ile haiwezi kuwa ya haki hata kidogo.

Hivi inawezekanaje mtuhumiwa akachunguzwa na watuhumiwa wenzake? Kwamba linalotuhumiwa ni jeshi, na wachunguzi wanakuwa wao. Hapa hakuna haki inayoweza kutendeka, isipokuwa ni kufichwa kwa ukweli na watuhumiwa kuachwa huru, hata kama kuna kila dalili kwamba walitenda uovu.

Ni kutokana na sababu hizo na kuongezeka kwa tuhuma dhidi ya Jeshi la Polisi, sisi katika Pambazuko tunaona wakati umefika sasa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kuunda Kurugunzi Huru ya Upelelezi kwa Polisi.

Tunapendekeza kwamba ikiwa Rais ataridhia kuundwa kwa kurugenzi hiyo, iwe ni sehemu ya watendaji walioko ofisini kwake – Ikulu, ili kuwepo na ufanisi na kuleta matokeo yanayotarajiwa kwa kila uchunguzi unaofanywa dhidi ya Polisi na watendaji wake.

Ni kurugenzi hiyo, ambayo itaundwa na watu weledi, wazalendo na wafia nchi ambao umma hautakuwa na chembe ya shaka juu ya tabia zao ndani ya utendaji wa kurugenzi hiyo maalum.

Dhamira kuu ya kurugenzi hiyo ni kuwa chombo chenye ufanisi, huru na kisichoegemea upande wowote katika uchunguzi na usimamizi ambacho kinatenda haki na kwa maslahi ya umma, huku kikidumisha viwango vya juu vya uadilifu na ubora.

Haya yakifanyika - nidhamu, haiba na sifa ya jeshi letu la Polisi inaweza kurejea na kuwa hasa walenzi wa mali na uhai wa Watanzania.

MAMA NA MWANA



Rais Samia Suluhu Hassan akimsikiliza Fatma Karume, mjane wa Rais wa Kwanza wa Zanzibar Sheikh Abeid Amani Karume (marehemu) mara baada ya kuhutubia na kuzindua Chama cha Wanawake Sekta ya Fedha Tanzania (Tawifa) Kizimkazi, Zanzibar Machi 14, 2024. (Picha na Ikulu).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko.tza@gmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



Mwisho wa maisha yetu huanza pale ambapo kila mtu anakaa kimya kwa mambo ya msingi yanapoonekana kuharibiwa. Kukaa kimya ni dhambi kubwa wakati wa kuonewa - Martin Luther King, mwanaharakati wa Marekani.

Tangazo

Tuchangie

Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako na wale wengine tuliowaomba kuchagia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**

**Mhariri Mkuu,
Oktoba, 2023**

Changia Pambazuko liendelee

WAJUMBE wa Bodi ya Uhariri, Mhariri Mkuu, wahariri, waandishi na watendaji wote wa gazeti la Pambazuko wameendelea kufuraha kusambaza habari, makala, safu, maoni, picha kwa miezi 15 bure kwa wasomaji wake.

Katika kipindi chote hicho cha kusambaza habari bila malipo, watendaji wa Pambazuko wamekuwa wakituma fedha, muda, ujuzi na rasilimali zingine kuhakikisha kila Jumatatu, gazeti hili linawafikia zaidi ya watu 500,000 duniani kote, bila malipo.

Ikumbukwe kwamba wazungumzaji wa lugha adhimu ya Kiwahili duniani kote; wanalitumia gazeti hili siyo kwa kupata habari tu, bali hata kusambaza kwa wengine kujifunza lugha hiyo inayokuwa zaidi kwa sasa.

Katika kipindi cha uhai wa gazeti hili - miezi 15, mengi mazuri yamepatikana, mbali na kukaza Kiwahili, kuhabarisha, kupaza maoni ya watu, lakini pia Pambazuko limeweza kusukuma watoto uamuzi, hasa serikali kuchukua hatua kwenye baadhi ya mambo ambayo yameweka wazi kwa umma. Gazeti hili limesaidia kuepusha majanga, kuponya majaraha na zaidi sana, kuunganisha jamii na kuchocha umoja na kumarisha amani.

Pamoja na mafanikio hayo makubwa - na bado yanaendelea, uongozi wa Pambazuko umepokea mawazo kwamba gazeti hili linazoe kusuzwa, lakini hasi kubalini na mawazo ya idadi kubwa ya wasomaji wake wanaopendekeza gazeti hivyo.

Lakini, uongozi huo umekubaliana na mawazo ya wachache kuruhusu umma kuanza kuchangia fedha kwa hiari ili kutoa mwanja kwa gazeti hili kuendelea kuufikia umma bure.

Sasa basi, endapo utapata kuchangia maendeleo na uhai wa Pambazuko, tafadhali tumia namba hizi kwa ajili ya mchango wako wa fedha.

Unaweza kutuma mchango wako na kuhimiza wengine kufanya hivyo kwa kuanzia shilingi 1,000 na hakuna ukomo wa kiwango cha juu; chochote kinapokelewa kwa shukrani na hakika tutatambua mchango wako. Kwetu sisi, hatuna kikubwa wala kidogo; yote ni mchango na ina thamani sawa ya "asante" kutoka kwetu.

Tuma mchango wako kutoka mtandao wowote wa simu yako ya mkononi - kwenda namba hii ya Lipa kwa TIGO na utatufikia; 6214500, Pia unaweza kuchangia kupitia namba ya Mpesa: 0744 768 263

Ukituma mchango wako kupitia simu, hakikisha jina linaandika: **Pambazuko Gazeti**. Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako - na wale wengine uliowaomba kuchagia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**.



Lulandala hebu acha ‘urongo’ bhana!

Na Igo AI

MZEE Tai ameomba apewe nambari ya simu ya mkononi ya Faki Lulandala, ambaye ni Katibu wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UCCM).

Sababu za kuisaka namba hiyo anadai ni kumfokea na eti anataka kumshikisha adabu Lulandala kwa kuwa anadai amesema uongo na kupotosha umma.

Mzee Tai anasema kwa kauli za Lulandala, anapanga kumfuata Rais Samia Suluhu Hassan ambaye ni mwenyekiti wa chama tawala (CCM) ili ashauriane namna ya kumpangia kazi nyingine “kijana” huyo kwa kuwa eti majukumu ya siasa yamemshinda.

“Kama hiyo namba hamtaki kunipa, naenda mwenyewe kwa mama, haiwezekani saa mbili zinapita umekosa namba ya huyo nani sijui; Lutandala au Lulanda, mtajua wenyewe, nasema leta namba,” akafoka Mzee Tai.

Mzee Tai alikuwa anamfokea mwandishi wake, huku akidai kucheleshwa kwa namba hiyo ni mbinu ya “kumlinda” Lulandala.

“Najua na wewe mwandishi ni walewale tu, hamjui lolote, wala hamjui nchi hii inaendeshwa namna gani, mwandishi gani wewe unakosa namna ya huyo kijana, wote ni walewale, naenda zangu mie kumuona mama,” alifoka tena.

Kufoka kote huko kwa Mzee Tai kulisababishwa na kukerwa na kauli ya Lulandala kwamba ukosefu wa ajira Tanzania ni matokeo ya kazi nzuri iliyoifanywa na CCM.

Lulandala akihojiwa na StarTV hivi karibuni alisikika akisema kuwa kuboreshwa kwa mazingira mazuri ya elimu na Rais Samia, kumefanya vijana wengi kupata uwezo wa kufanya kazi, lakini kwa kuwa ajira ni finyu, na wao ni wengi, ndiyo maana wanakuwa “mitaani wakizurura.”



Faki Lulandala

Mzee Tai akasema kauli hiyo ni dharau, na haikupaswa kuwekwa hadharani na kiongozi wa chama chake.

“Yaani sisi tunakaribia uchaguzi, huyu kijana analeta dharau za namna hiyo, hivi anajua siasa kweli au ana ajenda ya siri, kwanza huyu hata sijui ametokea wapi, sijawahi kumuona, simjui...”

... Wewe mwandishi niambie ametokea wapi huyu Lulandala, au ni kama wewe tu, sijui hata nani alikuleta kwangu, nakwambia kuleta namba ya simu unambwelamwela tu hapa, je, nikikutuma kumhoji Putin utaweza kweli wewe,” akaendelea kufoka.

Mzee Tai hakukerwa na hilo tu. Lipo jingine, kwamba Lulandala alitamka kwamba mikopo ya vijana inayotolewa na serikali inawafaidisha zaidi vijana wa CCM kwa kuwa ndiyo wengi na kwamba wanajielewa zaidi kuliko wale wa vyama vingine.

“Huyu kijana amenichefua sana, hili nalo la kuweka hadharani kwamba vijana wa chama chetu ndiyo wanapata zaidi mikopo kuliko wa Chadema na ACT – Wazalendo, kwanini amelitamka, huyu hafai maana hili ni jambo la ndani, nani kampa ruhusa kulitamka? Hafai kabisa,” akazomoka huku mate yakimtoka kinywani kama mvua.

Habari

Tanapa yajizatiti kukabili wanyama wakali

Na Mwandishi WETU

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa (Tanapa), limeweka mikakati ya kudhibiti wanyama waharibifu na wakali ili kulinda maisha ya binadamu na mali zao.

Moja ya mikakati hiyo kuhakikisha usalama wa watu wanaoishi jirani na hifadhi za taifa ni kutoa mafunzo kwa askari wa vijiji ili kudhibiti wanyama hao.

Askari hao wamepata mafunzo ya namna ya kudhibiti wanyama hao kabla hawajafika maeneo wanayoishi watu na kusababisha madhara na pia wanapokuwa wamevamia maeneo ya makazi ma mashamba.

Tayari askari 354 kutoka vijiji 39 wamepatiwa mafunzo hayo mahsusi.

Kamishna Mkuu wa Uhifadhi wa Tanapa (CC), Alhaj Mussa Kuji ameliambia Pambazuko kwamba katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita shirika limeshughulikia kwa wakati matukio 4,954 ya wanyamapori wakali na waharibifu yaliyoripotiwa.

Aidha, shirika pia limenunua mitambo 59 ya aina mbalimbali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo kama vile Benki ya Dunia (WB) na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF)kupitia Mradi wa Kuboresha Utalii Kanda ya Kusini (Regrow).

“Mitambo iliyonunuliwa kupitia mradi wa Regrow ni mashine mbalimbali, malori 17, bulldozers (tingatinga) mbili, motor grader tano, compactor tatu, low loader mbili, , excavator mbili, concrete mixers tano, matrekta saba, malori ya kubebea maji matano, magari ya sinema manne, magari ya kutolea elimu kwa wanafunzi na jamii matatu na malori ya kutengeneza magari matano,” amengeza.

Alhaj Kuji amebainisha kuwa shilingi



*Kamishna Mkuu wa Uhifadhi wa
Tanapa (CC), Alhaj Mussa Kuji*

bilioni 27.87 zilitumika kununua mitambo hiyo.

Pia mradi huo umeviwezesha jumla ya vikundi 138 kutoka katika vijiji vilivyo katika eneo la mradi kuanzisha miradi mbalimbali ya uzalishaji mali ikiwemo ufugaji wa nyuki, uchakataji wa viungo vya chakula na ufugaji.

“Jumla ya shilingi billion 2.4 zilitumika kuwezesha miradi ya uzalishaji mali. Pia, Benki za Kijamii za Uhifadhi yaani Cocoba 159 zilianzishwa kupitia mradi wa Regrow na kupewa fedha mbegu (mitaji) kiasi cha shilingi bilioni 1.453,” amesema Alhaj Kuji.

Aidha kupitia Regrow, Tanapa imetoa ufadhili wa masomo kwa wananchi ambapo jumla ya wanafunzi 1,051 kutoka vijiji 60 vinavyotekeleza mradi wa Regrow wamepatiwa ufadhili wa masomo wenye thamani ya shilingi bilioni 4.27 katika vyo mbalimbali vya kitaaluma hapa nchini.



Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com

Mezani kwa Chahali

Dkt Ndumbaro 'akaangwa' kila kona

MIONGONI mwa habari zilizotawala sana wiki iliyopita ni pamoja na kauli ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dkt. Damas Ndumbaro kuhusu kile alichaita "uzalendo kupitia soka."

Waziri Ndumbaro alinukuliwa akiamuru kwamba "Ukija Uwanja wa Taifa ukiwa umevaa jezi wa Mamelodi Sundowns, lazima utuoneshe passport (hati ya kusafiria) ya Afrika Kusini na ukiwa na jezi ya Al Ahly utuoneshe passport ya Misri, nje na hapo ukifanya fujo, Polisi watakuchukua ukapumzike kidogo utatoka baada ya mechi."

Amri hiyo ya Waziri Ndumbaro siyo tu ilipokelewa kwa hasira kubwa na Watanzania wengi, hususan kwenye mitandao ya kijamii, bali pia ilisababisha waziri huyo kuonekana kama kituko machoni mwa wengi, hasa washabiki wa vilabu vya Simba na Yanga.

Miongoni mwa masuala yaliyotatiza wengi kuhusu amri hiyo ya Dkt. Ndumbaro ambaye kitaaluma, ni msomi mwenye shahada ya uzamifu katika sheria, ni namna alivyoshindwa kutumia usomi wake kabla ya kuzomoka.

Wengi walitarajia kuwa usomi wake ungemuongoza vyema katika kushughulikia suala hilo.

Lakini, licha ya usomi wake, Dkt. Ndumbaro ambaye ni shabiki maarufu wa soka, na amewahi kuwa kiongozi wa klabu ya Simba ya Dar es Salaam, akazunguma kama "mjinga wa sheria."

Kwamba kwa usomi wake alitarajia kufahamu kwa kiasi kikubwa taratibu, sheria na kanuni zinazoongoza soka duniani.

Binafsi, amri hiyo ya Dkt. Ndumbaro imenikumbusha utekelezaji wa sera ya vijiji vya ujamaa iliyotokana na Azimio la Arusha la mwaka 1967.

Pamoja na malengo mazuri ya sera hiyo, moja ya sababu za msingi za kufeli



Dkt. Damas Ndumbaro

kwake ni matumizi ya mabavu badala ya busara.

Badala ya viongozi kuwashawishi wananchi kuhamia kwenye vijiji vya ujamaa, wao walitumia nguvu, na matokeo yake baadhi ya watu walipoteza ardhi na biashara zao na wengine kupelekwa maeneo yasiyokuwa na ardhi yenye rutuba kwa kilimo.

Kama ilivyokuwa kwenye utekelezaji wa sera hiyo, Dkt. Ndumbaro naye alitumia ubabe badala ya busara.

Angeweza kabisa kuwasihhi mashabiki wa Simba wasivae jezi za timu za kigeni zinazokuja Tanzania kuchuana na Yanga, sambamba na kuwasihhi mashabiki wa Yanga wasivae jezi za timu za kimataifa zinazokuja kuchuana na Simba.

Habari njema ni kwamba Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) limeliandikia barua Shirikisho la Soka Africa (CAF) kwamba hakuna mtu atakayetakiwa kuonesha hati ya kusafiria (passport) kabla ya kuingia uwanjani, na "kumuumbua" Waziri Ndumbaro.

Kichekesho ni kwamba siku chache zilizopita, Rais wa TFF, Wallace Karia aliongea na waandishi wa habari na kudai anaunga mkono amri ya Dkt. Ndumbaro. Kwa lugha ya mtaani, wanasema "Karia alimuungiza chaka Daktari Ndumbaro".

Habari

Aliyefungwa miaka 23 kwa ujangili atoroka

Mwandishi WETU

MFUNGWA Amos Bernard Mtinange, maarufu kwa jina la Meja, aliyekuwa anatumikia kifungo cha 23 kwa ujangili, ametoroka akiwa chini ya ulinzi, wilayani Babati, Manyara, Pambazuko linaeleza.

Mfungwa huyo ametoroka akiwa katika shamba la Magereza akifanya kazi chini ya usimamizi wa askari wenye silaha.

Alihukumiwa kifungo hicho Novemba mwaka Jana.

Mkuu wa Magereza Mkoa wa Manyara (RPO), Solomon Mwambingu amethibitisha tukio hilo jana na kusema – “kweli Meja ametoroka.”

“Tunazo hizo taarifa na suala hili linafanyiwa kazi, “ amesema mkuu huyo wa Magereza, huku akigoma kueleza mazingira ya Meja kutoroka.

Meja anadaiwa kutoroka Alhamisi ya wiki iliyopita akiwa na mfungwa mwingine ambaye alikamatwa na askari wa Magereza siku hiyohiyo.

Meja alikuwa “anateleza”

Taarifa za kutoroka kwa mfungwa huyo ambaye anaeleza na askari wa Mamlaka ya Usimamizi Wanyamapori (Tawa) ambao hatimaye Aprili 23, mwaka jana walikamatata - kuwa alikuwa mtata na “mtu anayeteleza” kila anapowekewa mitego ya kukamatata.

“Tunasikia mazingira ya kutoroka kwake yana utata mkubwa,” amesema ofisa mmoja wa Tawa, ambaye ameliomba Pambazuko lisitaje jina lake kwa sasa.

Meja alikuwa akisakwa kwa “udi na uvumba” na vyombo vya usalama kwa kuwa alikuwa mwindaji mkubwa wa twiga.

“Hizi taarifa zimenishangaza sana, tuliambiwa alitoroka akiwa na mwenzake mmoja ambaye tayari amekamatwa, yaani kazi yetu kubwa kumkaamta sasa imekuwa bure kabisa, eti ametoroka, huyu ni jangili mbobezi,” ameegeza.

Meja alifungwa miaka 23

Mahakama ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Wilaya ya Babati, Manyara, ilimuhukumu Meja kwenda jela miaka 23, baada ya kumtia hatiani kwa makosa mawili ya uhujumu uchumi; ujangili wa twiga na kuuza nyama za twiga kinyume cha sheria.

Meja alikamatwa April 20, mwaka 2023 saa kumi na moja jioni maeneo ya Mfulwang’ombe kwenye Kambi ya Samaki Kijiji cha Vilima vitatu, ndani ya eneo la hifadhi ya jamii ya wanyamapori ya Burunge, wilayani Babati, Manyara baada ya kusakwa muda mrefu kutokana na kujihusisha na ujangili wa wanyamapori, hasa twiga.

Akisoma hukumu hiyo, hakimu wa mahakama hiyo, Victor Kimario alisema mahakama ilimtia hatiani Meja baada ya kujiridhishwa pasi na shaka kuwa alikuwa akijihusisha na ujangili wa twiga.

Kabla ya hukumu hiyo, Meja aliomba mahakama kumpunguzia adhabu kwani ana familia inamtegemea.

Hata hivyo, wakili wa serikali, Benedict Mapunda na mawakili wa Tawa, Getrude Kariongi na Shahidu Kajwagya, walipinga kupunguziwa adhabu mtuhumiwa huyo.

Wakili Kariongi alisema kesi inayomkabili mtuhumiwa huyo ni ya uhujumu uchumi na kwamba amekuwa akifanya ujangili kwa muda mrefu ni kuuwa twiga ambao ni kivutio cha utalii nchini.



Meja baada ya kukamatwa mwaka jana



Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

Ni aibu kufadhiliwa matundu ya vyoo

Na Rashid MTAGALUKA

NI JAMBO la kawaida mtu binafsi, familia na jamii kwa ujumla kuomba kusaidiwa chochote baada ya juhudi za ngazi husika kufika mwisho katika utatuzi wa changamoto.

Kwa mfano, sioni kama kuna shida mtu kumuomba ndugu yake pesa kwa ajili ya kumalizia ada ya kijana wake ili aruhusiwe kufanya mitihani chuoni.

Na wala hakuna tatizo kwa familia moja kuomba msaada kwa jamii iliyowazunguka baada ya kukumbwa na maafa ya kuunguliwa, mafuriko na kadhalika kwa kuwa jambo hilo ni la dharura linalohitaji utu!

Hata hivyo, hakuna udharuru wa familia huru yenye watu wenye uwezo wa kufanya kazi, ikabweteka na kujigeuza ombaomba ikisubiri misaada ya jirani ili iweze kuishi.

Kwamba inastaajabisha familia kama hiyo ikitokea popote pale duniani, licha ya kwamba ndani ya nyumba yao kuna kila nyenzo inayoweza kuwasaidia kupata riziki wakaishi, lakini bado wanangoja mfadhili awalettee pilau!

Sisi Tanzania kwa kuwa ni nchi huru iliyojaa rasilimali tele pamoja na viongozi wazalendo, wakiongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, tunapaswa tufanye kila liwezekanalo kujiondoa kwenye mfano wa familia kama hii.

Inasikitisha sana na sijui hii inatokana na nini hasa, kila mara tumekuwa tukisikia kelele za shule zetu nyingi za umma, katika baadhi ya halmashauri hapa nchini, zina upungufu wa matundu ya vyoo.

Aidha, tumewahi kusikia baadhi ya shule za msingi na hata za sekondari, walimu wake wanalazimika kupanga foleni moja na wanafunzi kwenda



Vyoo vya msaada

maliwatoni kutokana na uhaba wa matundu ya vyoo.

Hivi tunawezaje kubana bajeti zetu na kuchangishana thumni thumni na hatimaye kujenga shule zetu wenyewe, halafu suala la matundu ya vyoo tsubiri waje kutujengea wafadhili kutoka nje ya nchi kama vile vyoo ndivyo vyenye gharama kubwa kuliko majengo ya shule?

Matahalan, mimi nahisi kichefuchefu nikifika mahala nikakuta vyoo vipya vya shule na pembeni kuna bango kubwa linaeleza ujenzi wa vyoo hivyo umefadhiliwa na watu wa nchi fulani huko ughaibuni!

Nimekuwa nikijiuliza sana bila kupata majibu kwamba, watu wa nchi hiyo wana maana gani kukubali kusaidia kujenga vyoo kwenye baadhi ya shule zetu, halafu wakaweka bango kwamba ujenzi huo wametusaidia wao?

Yaani uwe na rafiki yako umuombe faraghani akusaidie nguo nzuri ya kuvaa ukiwa na safari au sherehe, yeye kwa kuwa anajiweza kiuchumi akakushonea suti maridadi kwelikweli na nyuma ya suti akaweka lebo yenye maandishi makubwa kwamba suti hiyo umesaidiwa na huyo rafiki yako!

Rashid Matagaluka ni mwandishi wa habari anapatikana kwa simu namba 0784 438546 au Barua pepe:mtagaluka@gmail.com

Habari

Hadithi za dini kusaidia Mahakama

Na Mwandishi WETU

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Hamis Juma, amesifia kazi iliyofanywa na mwandishi wa kitabu cha tafsiri ya hadithi 40 za Imam Nnawawy, akibainisha kuwa kitasaidia watumishi wa Mahakama kutoa haki.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa kitabu hicho jijini Dar es Salaam wiki iliyopita, Jaji Juma aliwataka Watanzania kukisoma kitabu hicho ili kujiongezea maarifa kwenye maeneo mbalimbali, ikiwemo haki, amani na kumjua Mungu.

Prof. Juma alisema kuwa kitabu hicho siyo tu kina manufaa makubwa katika eneo la utoaji haki, ambalo amelisimamia kwa miaka mingi, bali pia katika maisha na kazi za kila siku anazozifanya binadamu.

“Kitabu hiki ni msingi wa mambo mengi katika maisha yetu, kazi zetu za kila siku na hadithi hizi zitatusaidia sana sisi tunaofanya kazi za utoaji haki katika kuweka msingi wa kuelewa sheria, sheria ambayo inajengwa katika misingi ya imani inakuwa na nguvu zaidi kuliko ambayo inatengenezwa kwa shuruti,” alisema.

Kitabu hicho kimeandikwa na Sheikh Issa Othman Issa.

Jaji Mkuu amebainisha kuwa mafunzo yanayotolewa kupitia hadithi 40 zilizoelazwa katika kitabu hicho, iwapa yatazingatiwa ipasavyo, matukio ya uvunjifu wa sheria na migogoro miongoni mwa wanadamu yangepungua.

Waziri Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, ambaye alihudhuria hafla hiyo alitoa mwito kwa kitabu hicho kuwekwa kwenye mfumo wa sauti ili kuwawezesha watu wengi zaidi kukiulewa.

“Kitabu hiki kikiwa katika mfumo wa sauti mtu anaweza kukisoma akiwa anaendesha gari au akiwa anapika au



Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Hamis Juma (katikati) akikata utepe kuashiria uzinduzi wa Kitabu cha Hadithi 40 za Imam Nnawawy. (Picha na Mpigapicha Wetu).

wakati anapumzika, lakini anaona uvivu kushika kitabu na kukisoma moja kwa moja,” alisema.

Alimpongeza mwandishi wa kitabu hicho kwani alichokifanya ni baraka kubwa kwa nchi na mtu mmoja mmoja ambao watapata maarifa ya kumjua Mungu kupitia kitabu hicho.

Alihimiza watu wengine kutunga vitabu vya namna hiyo kama njia ya kukabiliana na wingi wa taarifa za kupotosha ambazo zimejaa mitandaoni hivi sasa.

“Kwa bahati sasa mitandaoni kumejaa taarifa, lakini kwa bahati mbaya nyingi ya taarifa hizo ni za kupotosha na hazitusaidii. Akipatikana mtu akaweka hata kwa sekunde moja taarifa zitakazotusaidia ni vyema tukamuunga mkono mtu huyu na tumsaidiane kupaza sauri,” alisema Nnauye.

Hafla ya uzinduzi wa kitabu hicho ilihudhuriwa na viongozi kadhaa wa Mahakama ya Tanzania, akiwemo Jaji wa Mahakama ya Rufani, Amour Khamis na Naibu Msajili wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kifungu Kariho. Alikuwapo pia Jaji Kiongozi Mstaafu, Amir Manento.

Sweden 'yanogewa' mradi wa SGR

Na Mwandishi WETU

SWEDEN imeamua kuongeza fedha ili kuendeleza mradi wa kujenga reli ya kisasa (SGR) kati ya Dar es Salaam na Morogoro, imefahamika.

Akizungumza jijini Dodoma hivi karibuni katika mazungumzo yake na Waziri wa Fedha, Dkt. Mwiguklu Nchemba, Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Maendeleo ya Kimataifa na Biashara ya Nje wa Sweden, Diana Janse, alisema nchi yake ipo tayari kutoa fedha zaidi ili kuendelea ujenzi wa mradi huo.

Katika mazungumzo hayo alisema kuwa Sweden ina nia ya kutoa zaidi ya dola za Marekani milioni 580 (shilingi trilioni 1,484,800,000,000) kwa ajili ya ujenzi wa kipande cha tatu na cha nne cha SGR.

"Tunashukuru sana kwa sababu huu ni mradi wa kimkakati, ni mradi wa kikanda ambao utasaidia siyo tu Tanzania, bali utasaidia pia nchi jirani zikiwamo Uganda, Burundi, DRC pamoja na majirani wengine," alisema Dkt. Nchemba.

Alibainisha kuwa ushiriki wa Sweden katika mradi huo ni jambo linalowagusa Watanzania na daima wataendelea kukumbuka hilo.

Dkt. Nchemba alisema kuwa ili kutolewa fedha hizo kwa ajili ya ujenzi wa kipande cha tatu na nne katika mradi huo jambo lililosalia kukamilishwa ni masuala ya mazingira, ambayo ni masuala ya msingi katika utoaji wa fedha kutoka Sweden.

Alisema Wizara ya Fedha, Ofisi ya Makamu wa Rais na Shirika la Reli Tanzania (TRC) watajitahidi kukamilisha jambo hilo ndani ya muda mfupi ujao ili kuwzesha kutolewa kwa fedha hizo ili kipande hicho cha reli ya kisasa nacho kijengwe.

Aidha, katika mazungumzo hayo



Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Maendeleo ya Kimataifa na Biashara ya Nje wa Sweden, Diana Janse,

waziri huyo wa Sweden alimweleza Dkt. Nchemba kuwa nchi yake inaandaa mkakati mpya wa ushirikiano kati ya nchi hizo mbili unaolenga kuongeza ushirikiano katika maeneo ya uchumi na biashara.

Mradi wa SGR unahusisha ujenzi wa mtandao wa reli ya kisasa yenye urefu wa kilometa 2,561 ukiunganisha mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma, Katavi na nchi jirani za Rwanda, Burundi na DRC.

SGR ni reli ya kisasa na ya kwanza Afrika Mashariki na Kati itakayokuwa na uwezo wa kupitisha treni zitakazoendeshwa kwa nishati ya umeme na yenye mwendo kasi unaofikia kilometa 160 kwa saa.

Kuhusu mkakati mpya wa ushirikiano, Dkt. Nchemba aliahidi kuwa Tanzania itashiriki kikamilifu katika kufanikisha mkakati huo na kuwakaribisha wawekezaji kutoka Sweden kuja kuwekeza nchini.

Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Maendeleo ya Kimataifa wa Sweden, alisema kuwa nchi yake inatambua kuwa mradi wa SGR ni moja ya miradi ya kipaumbele kwa Tanzania na kwamba nchi yake iko tayari kushiriki katika ujenzi wa mradi huo.

Makala

Biashara ya hewa ya ukaa, mkondo mwingine wa ukoloni mamboleo

Na Mwandishi WETU

NCHI kadhaa za Afrika “zimejawa furaha na zinarukaruka kwa bashasha” baada ya kuwa na uhakika wa kupata mabilioni ya dola za Marekani kupitia biashara ya hewa ya ukaa.

Lakini kimsingi wanachofurahia ni kifo.

Iko hivi; nchi zilizoendelea zitakuwa zinatoa fedha (kama fidia) kwa nchi masikini ambazo zinaendesha miradi ya kimazingira inayosaidia kupunguza kiwango cha hewa ya ukaa angani.

Yaani nchi tajiri zitaruhusiwa kuendelea na shughuli zao zinazozalisha kiasi kikubwa cha hewa ya ukaa kama kawaida, lakini ili kuzuia hewa hiyo isiendelee kuhatarisha maisha duniani, basi wataumia sehemu ya faida wanayoipata kutokana na shughuli zao, kuzilipa nchi masikini ambazo zina miradi inayosaidia kupunguza hewa ukaa angani.

Maana yake ni kuwa nchi zilizoendelea zitaachwa ziendelee kuzalisha hewa ya ukaa na nchi masikini zitakuwa zinalipwa ili kusafisha hewa hiyo chafu inayozalishwa na nchi tajiri.

Lakini ili nchi masikini ziweza kufaidi fedha hizo za biashara ya hewa ya ukaa zinapaswa kutimiza vigezo na masharti kadhaa.

Vigezo na masharti hayo vinapangwa na nchi tajiri!

Tena ili nchi masikini ziweza kupata fedha hizo za biashara ya hewa ya ukaa inabidi miradi yao ifanyiwe tathmini kuona kama inakidhi masharti na vigezo vilivyowekwa.

Tathmini hiyo inafanwya na taasisi chache sana duniani ambazo zote zimeanzishwa, zinaendesha na zipo kwenye nchi tajiri!



Matokeo ya ukame mkali

Lakini nchi masikini zinashangilia mpango huu kwa sababu zenyewe zinafikiria tu zile dola watakapopata bila kujiuliza ni nini kinatokea kwenye hali ya hewa nchi tajiri zinapoachwa ziendelee kuzalisha hewa ya ukaa?

TFS yatoa neno

Hii siyo hali inayopaswa kuachwa iendelee hivi hivi. Kama hali itaachwa iendelee hivi hivi, itakuwa ni ndoto kwa dunia kupunguza ongezeko la joto duniani kwa sababu hewa ya ukaa itaendelea kuzalishwa.

Hivyo, jambo la muhimu ni kuhakikisha kuwa kiwango cha hewa ya ukaa kinachozalishwa kinapunguzwa na upunguzwaji wake usitokane na miradi katika nchi masikini, bali kupunguzwa kwa shughuli zinazozalisha hewa ya ukaa katika nchi tajiri kama ambavyo Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Huduma za Misituta Tanzania (TFS), Prof. Dosantos Silayo alivyodokeza hivi karibuni.

“Biashara hii (ya hewa ya ukaa) inapaswa kufanyika kwa namna ambayo itafanikisha lengo lake kuu; la kupunguza kiwango cha hewa ya ukaa inayozalishwa.

Biashara ya hewa ya ukaa

Inatoka Uk. 12

Biashara inapaswa kuhakikisha kila upande unanufaika na maslahi ya kila upande yanazingatiwa,” anasema Prof. Silayo.

Anasisitiza kuwa biashara hiyo haitakuwa na maana iwapo inazifanya baadhi ya nchi ziendelee kuzalisha hewa ya ukaa huku nyingine zikitumika kama vyombo vya kusafisha hewa hiyo inayozalishwa.

Dola zamwagwa kwa Tanzania

Prof. Silayo anayasema hayo wakati ambao Tanzania nayo ni moja ya nchi ambazo tayari zimeshaanza kunufaika na biashara hiyo.

Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Mazingira, Dkt. Suleiman Jafo, amenukuliwa hivi karibuni akisema kuwa Tanzania inajipanga kuingiza kiasi cha dola bilioni moja kupitia biashara ya hewa ya ukaa.

Akizungumza mwezi uliopita, Dkt. Jafo alisema tayari miradi 39 yenye sifa za kupata fidia kupitia biashara ya hewa ya ukaa imeshasajiliwa huku miradi 12 kati yake ikiwa imepatiwa kibali cha kuendelea.

Akieleza uwezekano wa Tanzania kuanza kufaidi dola hizo, Jafo alieleza kuwa Wilaya ya Tanganyika inatarajiwa kupokea kiasi cha dola milioni 1.6 (shilingi bilioni 1.4 wakati wilaya za Mbulu na Kiteto zikiwa zimeshapokea dola milioni 2.1 (shilingi bilioni 4.8).

Fedha hizi zimelipwa au zitalipwa moja kwa moja kwa halmashauri hizo kupitia miradi ambayo inahifadhi mazingira.

“Hii inaonesha kuwa Tanzania ina fursa nzuri ya kutengeneza fedha kupitia biashara ya hewa ya ukaa,” alisisitiza Dkt. Jafo.

Hata hivyo, wakati Waziri Jafo akijinasibu kuwa nchi ipo tayari kwa



Profesa Silayo

biashara hiyo, hakuna ushahidi wa kitakwimu unaoonesha hiyo.

Mathalan, hadi hivi sasa hakuna takwimu zozote zinazoonesha Tanzania ina uwezo gani wa kupunguza kiwango cha hewa ya ukaa wala hakuna takwimu zinazoonesha Tanzania imepunguza kiasi gani cha hewa ya ukaa licha ya kupokea mabilioni hayo ya fedha.

Kuhusu hilo Prof. Silayo anasisitiza kuwa iwapo dunia inataka kuondokana na tishio la kuongeza kwa joto, basi kinachopaswa kufanyika ni kuhakikisha kuwa uzalishaji wa hewa ya ukaa unapunguzwa hadi viwango vilivyokubaliwa.

Alibainisha kuwa mtindio wa kuziacha baadhi ya nchi ziendelee kuzalisha hewa hiyo hatari, huku nchi nyingine zikitumika kama chujio la kuiondoa hautafanikiwa kwa sababu hakuna uhakika kuwa kiasi cha hewa kitakachoondolewa kupitia miradi hiyo kitaendana na hewa iliyozalishwa.

Afrika, licha ya kuzalisha kiasi kidogo sana cha hewa ya ukaa, lakini ndilo bara linaloathirika zaidi ya majanga

Makala

Biashara ya hewa ya ukaa

Inatoka Uk. 13

yanayotokana na mabadiliko ya tabia nchi kutokana na kuongezeka kwa joto duniani.

Majanga kama vile vimbunga, mafuriko, ukame, kuongezeka kwa kina cha bahari, mvua zisizo na uhakika, ni kati ya mambo yaliyoliandama Bara la Afrika katika miaka ya hivi karibuni.

Kwa kiasi kikubwa mambo haya yote yanatokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Uzalishaji vs upunguzaji

Kwa mujibu wa Benki ya Dunia, mwaka 2019 dunia ilizalisha tani milioni 48 za hewa ya ukaa, huku kiasi kikubwa cha hewa hiyo kikizalishwa na nchi zilizoendelea na zile zenye idadi kubwa ya watu.

Kwa wastani kila mtu anazalisha takribani tani 6.2 za hewa ya ukaa kwa mwaka, lakini kuna baadhi ya nchi ambazo zinazalisha mara tatu ya wastani huu.

Kwa mujibu wa takwimu za Benki ya Dunia, kiasi cha uzalishaji wa hewa ya ukaa katika nchi zilizoendelea ni mara mbili zaidi (tani 9.9 ya wastani wa dunia wa tani 4.6) huku nchi zinazoendelea zikizalisha wastani wa tani 1.7 ikiwa ni nusu ya wastani wa dunia na nchi masikini zikizalisha kiasi kidogo sana cha wastani wa tani 0.3.

Nchi zinazotajwa kuzalisha hewa ya ukaa kwa wingi ni China (asilimia 30) na Marekani (karibu asilimia 14).

Hata hivyo, ukipima uzalisha wa hewa ya ukaa kwa wastani wa idadi ya watu nchi zinazozalisha mafuta za Qatar, Bahrain na Kuwait ndizo zinashika nafasi ya juu.



Kwa wastani, nchi masikini kutoka Afrika, Asia, Marekani (ya Kati na Kusini) huzalisha kiwango kidogo sana cha hewa ya ukaa, lakini kutokana na uwezo wao mdogo kiuchumi, ndizo zinaathika kwa kiasi kikubwa kutokana na madhara ya mabadiliko ya tabia nchi.

Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) linabainisha katika moja ya tafiti zake kuwa ongezeko la nyuzi moja ya joto katika nchi ambayo wastani wa joto kwa mwaka ni nyuzi-joto 25 kama ilivyo kwa Bangladesh au Haiti, kunapunguza pato la wastani la mwananchi wake kwa asilimia 1.5, kiwango ambacho kinakadiriwa kuwa kitaongezeka hadi asilimia kumi mwishoni mwa muongo huu iwapo dunia itashindwa kupunguza uzalishaji wa hewa ya ukaa.

IMF inasema ongezeko la joto duniani litaathiri uchumi katika nchi masikini kupitia kushuka kwa uzalishaji katika kilimo, kushuka kwa tija ya wafanyakazi, kushuka kwa uwekezaji na kuongezeka kwa matatizo ya kiafya.

Takribani asilimia 60 ya watu duniani hivi sasa wanaishi katika nchi hizo masikini ambazo hazina uwezo mkubwa wa kukabiliana na mabadiliko ya hali hewa.



Tangaza na **Pambazuko**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.

Kwa bei nafuu sana

0744 768 263 au
Barua- Pepe; info@pambazuko.tz

Habari

Vyombo vya habari huru zaidi - Serikali

Na Mwandishi WETU

SERIKALI ya awamu ya sita, “imejipiga kifua” kwamba imefungua milango kwa waandishi wa habari kuandika kwa uhuru.

Kwamba tangu Rais Samia Suluhu Hassan aingie madarakani, Machi 2021, kumekuwa na uhuru mkubwa wa kujieleza na kutoa maoni kwa njia mbalimbali - kupitia vyombo vya habari na majukwaa mbalimbali ya kuhabarisha umma.

Jana, wakati akieleza mafanikio ya uongozi wa Rais Samia ndani ya miaka mitatu ya uongozi wake, Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi alisema kwa kuthamini uhuru wa vyombo vya habari, kwa amri ya rais, aliyafungulia na kuyapa leseni mpya za uchapishaji magazeti ya Mwanahalisi, Mawio, Mseto, na Tanzania Daima yaliyokuwa yamefungiwa kwa muda mrefu.

Matinyi akaeleza kuwa wakati serikali ya awamu ya sita inaingia madarakani Machi, 2021 kulikuwa na machapisho 266. Kutokana na uhuru uliopo sasa, jumla ya machapisho 351 yana leseni – ongezeko la machapisho 87.

Alisema kuwa baada ya Sheria ya Huduma za Habari kupitishwa mwaka 2016, wadau walikuwa na maoni tofauti ambayo yaliyotaka mabadiliko kadhaa ili kuweka wigo mpana kwa vyombo vya habari kufanya kazi zao kwa uhuru zaidi.

“Wizara kwa kushirikiana na wadau ilifanya mapitio ya Sheria ya Huduma za Habari Sura ya 229 na kanuni zake na hatimaye ikarekebishwa Juni 2023 na baada ya serikali kupokea maoni ya wadau, waziri akizisaini kanuni mnamo Januari 2024,” alisema.

Kwamba serikali pia inaendelea na kukamilisha hatua muhimu za utekelezaji wa sheria hiyo ikianzia na uundaji wa Bodi ya Ithibati ambayo itawezesha uundaji wa Baraza Huru la Vyombo



Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi

vya Habari na Mfuko wa Mafunzo kwa Waandishi wa Habari.

Matinyi alisema marekebisho haya yamewaondoa wanahabari katika makosa yanayohusiana na kashfa za kijinai, makosa ambayo kwa kawaida yanaangukia katika utaratibu wa mashauri ya madai.

Vilevile, adhabu kwa wamiliki wa mitambo ya uchapishaji, ambao katika hali ya kawaida, hawana uwezo wa kudhibiti maudhui yanayochapishwa katika mitambo hiyo ya uchapishaji zimeondolewa.

Pia Matinyi alieleza kuwepo kwa maboresho yanafanyika kutokana na maoni ya wadau wa sekta ya utangazaji ili iweze kuendana na wakati.

Akizungumzia jitihada za kuhakikisha sehemu kubwa ya Tanzania inafikiwa na mawasiliano ya simu, Matinyi alisema serikali pia kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) imefanikiwa kupata shilingi bilioni 126 kwa ajili ya ujenzi wa minara mipya 758 katika kata 713 ili kuwezesha wananchi milioni 8.5 kupata huduma za mawasiliano; na kupandisha hadhi minara 304 kutoka 2G kwenda teknolojia ya 3G na 4G.

Alisema pia kuwa Mkongo wa Taifa umeongezewa mtandao wake kwa ujenzi ambapo sasa unafikia wilaya 67 nchini kutoka 36 mwaka 2020/21.

Barua Kutoka Roma

Tukemea ufisadi ndani ya familia kwanza

Na Frt. Benedict Msoffe,
Roma, Italia

JAMII ndiyo hazina ya nchi. Kutoka humo nchi hupata viongozi wa kisiasa na hata wa kidini, wataalamu, wafanyakazi, wazazi, vijana na kila aina ya raia itakayokuwa nao. Manazuoni Abraham J. Heschel, mwenye asili ya Uyahudi na mchambuzi, anaeleza kazi ya manabii katika kitabu chake, “The Prophets.”

Uchambuzi wake unaangazia hasa hali ya kijamii na kisiasa ya Israeli wakati wa unabii wa manabii wa kwanza kuweka kazi zao katika maandishi (Amos, Hosea, Isaya na Mika).

Mmoja wa manabii hao ambaye unabii wake ulitawaliwa na hisia kali za kukemea na kuonya dhidi ya uasi wa watu alikuwa Hosea.

Katika mambo mengi, Nabii Hosea alipigia kelele ufisadi.

Kwa Hosea, ufisadi ni ishara ya kwamba jamii nzima imeoza kabisa kuanzia katika “mizizi hadi matawi.”

Hosea alionya kuwa ufisadi haukuwa tu katika mahali pa juu, bali kila mtu katika nafasi yake alitekeleza ulaghai uliokuwa ukijidhihirisha kwa namna tofauti-tofauti.

Ni kama inavyoonekana leo, ambapo watoto na vijana kidogo kidogo hujifunza kutokana na uhusiano ndani ya familia, kutokuaminina, kutokuwepo uadilifu na kuwajibika.

Na hapo endapo ndani kuna shida, basi watoto hujifunza mambo mabaya.

Hii hukumbusha habari ya miaka kadhaa iliyopita wakati wa mazishi ya Askofu Anthony Mayala wa Jimbo Katoliki Mwanza. Katika ibada ya mazishi yake walikusanyika watu wa kila hadhi.

Walikuwepo viongozi wa serikali pamoja na dini na katika salamu kadhaa, wengi waliopata nafasi walimzungumzia Askofu Mayalla kwamba alikuwa akikemea ufisadi kwa nguvu zake zote.

Ibada iliadhimishwa na Kardinali Pengo ambaye pamoja na mengine yote, aligusia vita dhidi ya ufisadi katika mahubiri yake.

Aliwauliza waliokuwa wamehudhuria swali; “tunapokemea sana ufisadi ni kwanini tunafanya hivyo?” Je! Ni kwa sababu tunauchukia kabisa ufisadi kwa moyo wetu wote. Je, tukipewa sasa hivi nafasi waliyonayo hao wanaofanya ufisadi ufisadi, utakoma?

Maswali hayo ya Pengo yanagusa kabisa jamii, ambayo ukiangalia wengi wanaopinga ufisadi kwa maneno makali, endapo watapata nasi, wanaweza kuwa vinara wa ufisadi.

Mifano ipo mingi yenye kuonesha jamii, inaweza kuwa sehemu kubwa ya kuubeba ufisadi, hata kama inaonekana ikiupinga hadharani.

Kipo kisa kinachobeba taswira hii ambacho kinasimuliwa na Biblia. Katika kile kisa cha mwanamke mzinifu aliyefikishwa mbele ya Yesu katika Injili (rej. Yohane 8:1 – 11).

Wanajamii wale walimkamata mwanamke kwa kumtuhumu dhambi, na kumpeleka kwa Yesu ili akahukumiwe, na walikuwa tayari na mawe kwa ajili ya kumpiga hadhi kufa endapo Yesu atatamka hukumu.

Basi, wakamkabidhi kwa Yesu, walitengeneza duara huku tayari kwa kumpiga mawe, Yesu, akawasikiliza, baadaye akainama kuandika kitu ardhini.

Alipomaliza kuandika, akawauliza – “nani asiyekuwa na dhambi kati yenu ili awe wa kwanza kurusha jiwe kumpiga mwanamke.”

Badala ya kujibiwa, wanaume wote waliomleta mwanamke yule “waliyeyuka” na kutokomea na ndipo Yesu akatamka kwa mwanamke; “nenda zako, usitende dhambi tena.”

Michezo

Uwanja wa Samia sawa, lakini uko wapi wa Mohammed VI?

Na Mwandishi WETU

SERIKALI imetangaza kuingia mkataba na kampuni kutoka China kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa michezo wa kisasa katika Jiji la Arusha.

Kwa mujibu wa Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo, uwanja huo ambao utakuwa na thamani ya shilingi bilioni 286, ni moja ya miundombinu inayojengwa kwa ajili ya michuano mikubwa ya soka ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon).

Tanzania, Kenya na Uganda ndiyo wenyeji wa fainali za michuano hiyo itakayofanyika mwaka 2027.

Waziri wa Sanaa, Utamaduni na Michezo, Dkt. Damas Ndumboorame amesema wamepanga kuupa uwanja huo jina la Rais Samia Suluhu Hassani, endapo kiongozi huyo wa Tanzania ataafiki.

Uwanja huo unaojengwa katika kata ya Olmoti, mkoani Arusha katika eneo lenye ukubwa wa ekari 36.1, utakuwa na uwezo wa kuchukua watazamaji 30,000 utakapokamilika.

Kwa watu waliokuwa wana shaka kuhusiana na dhamira ya serikali kuwa mwenyeji wa Afcon 2027, hatua hii ni

uthibitisho kuwa serikali imedhamiria.

Imeelezwa kuwa katika Afcon 2027 Tanzania itashirikiana na Kenya na Uganda kuwa wenyeji katika kile kinachoitwa 'Pamoja Bid.'

Hii ina maana kuwa baadhi ya mechi za mashindano hayo zitachezwa Tanzania wakati mechi nyingine zikichezwa Kenya na Uganda.

Hapa nchini tumeelezwa kuwa mechi zitafanyika katika majiji ya Dar es Salaam, Arusha na Zanzibar. Kwa kuwa Zanzibar tayari ina uwanja wa kisasa, New Aman Complex ambao umefanyiwa ukarabati mkubwa, ili kuiwezesha Arusha nayo kuwa mwenyeji wa fainali hizo, ndipo uamuzi wa kujenga uwanja wenye hadhi hiyo ukafanyika.

Watu wengi wameisifia serikali kwa hatua hii na kwa hakika serikali inastahili pongezi hizo.

Lakini, wakati tunatoa pongezi tunapaswa kuangalia nyuma na kujiuliza kwa nini mji mkuu wa nchi, yaani Dodoma, siyo sehemu ya majiji yatakayokuwa wenyeji wa mechi hizo za Afcon 2027?

Jibu linaweza kuwa ni kwa sababu jiji

Endelea Uk. 19



Mchoro unaonesha mwonekano wa uwanja wa kisasa wa michezo utiopianwa kujengwa jijini Arusha.

Uwanja wa Samia sawa,

Inatoka Uk. 18

hilo halina uwanja wenye hadhi.

Lakini, miaka michache tu iliyopita nchi iliishtuliwa na kishindo cha tangazo la kuwa Mfalme Mohammed VI wa Morocco ameipa Tanzania msaada wa uwanja mkubwa wa kisasa wa michezo na serikali ikatumbia kuwa uwanja huo utajengwa katika Jiji la Dodoma.

Hata hivyo, tangu kutolewa kwa tangazo la msaada wa uwanja wa michezo, hakuna kingine cha maana kilichotokea, hakuna maelezo kuhusiana na uwanja huo hadi hivi sasa.

Tunakumbuka kuwa rais wa awamu ya tano, Dkt. John Magufuli alitangazia umma wa Tanzania kuwa alimuomba Mfalme Mohammed VI msaada wa kujenga uwanja wa kisasa, naye akakubali.

Ilielezwa wakati huo kuwa ujenzi wa uwanja huo wa kisasa utagarimu kati ya shilling bilioni 174 na 228.

Sifa zikamwagwa kwa Dkt. Magufuli wakati huo ikielezwa kuwa iwapo hilo litatimia kiongozi huyo atakuwa amecha alama kubwa kwa taifa.

Wale waliokuwa mashabiki wa utawala wa wakati huo walisema hayo kwa lengo la kutaka kumlinganisha na hatimaye kumuweka Dkt. Magufuli juu ya rais wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa, ambaye alifanikisha ujenzi wa uwanja mkubwa wa kisasa wa michezo jijini Dar es Salaam ambao umepewa jina lake.

Hadi wakati huo, uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam unabakia kuwa ni moja ya viwanja vikubwa vya michezo Afrika Mashariki.

Lakini, kwa bahati mbaya Rais Magufuli alifariki dunia mwaka 2021 wakati uwanja huo haujajengwa.

Leo tunaadhimisha miaka mitatu tangu kufariki kwake bado hakuna dalili za wazi kuwa uwanja huo utajengwa.

Kitu cha kushangaza zaidi serikali iliyojengea uwezo wake wa ndani kujenga uwanja wa kisasa wa michezo imeamua kujenga uwanja huo jijini

Arusha na siyo Dodoma, ambako tayari kulikuwa na ahadi ya kujenga uwanja huko.

Kwa nini serikali haikuamua kujenga uwanja huo wa kisasa jijini Dodoma uwe mbadala wa ule wa Mfalme wa Morocco bado kitaendelea kuwa kitendawili ambacho tutakaa tukisubiri jibu lake.

Labda watu wanaweza kusema kuwa kwa kuwa Dodoma ilishaahidiwa uwanja na ahadi hiyo bado ipo, basi ni vyema kupeleka uwanja huo mpya mahali pengine.

Kama ni hivyo kwa nini wakati huo ambapo ujenzi wa uwanja uliaahidiwa Dodoma ukiwa unasuasua serikali isijenge uwanja wake huko Dodoma na utakapokuja huo wa msaada, kama kweli utakuja, ukajengwe Arusha?

Uamuzi wa kujenga uwanja Dodoma ungelipa jiji hilo mwenyeji wa makao makuu ya nchi hadhi ya kuwa pia mwenyeji wa mechi za Afcon 2027, ambalo ni tukio kubwa la kimichezo barani Afrika.

Tutakapokuwa tunauona uwanja huo wa Arusha ukiinuka, kwa hisia kali, tutakuwa tunajiuliza hivi ile ya ahadi ya Mfalme wa Morocco kujenga uwanja wa soka jijini Dodoma iliishia wapi?

Tukatapooni uwanja wa Arusha tutakuwa tunajiuliza hivi ni Mfalme Mohammed VI alimdanganya Dkt. Magufuli au Magufuli alitudanganya Watanzania?

Wakati tutakapokuwa tunashereheka kukamilika kwa uwanja wa Samia Suluhu Hassan, jijini Arusha tutakuwa tunawaza kwa hisia kali kuwa pengine Mfalme Mohammed VI wa Morocco alishatoa pesa, lakini fedha hizo zimepotelea hewani!

Na tutakuwa na haki ya kujiuliza maswali hayo kwa sababu ni miaka minane sasa imepita tangu ahadi hiyo itolewe, lakini hakuna dalili za utekelezaji wake.

Upo wapi uwanja wa Mohammed

Tulia ndani Geneva



Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) na Spika wa Bunge la Tanzania, Dkt. Tulia Ackson, amefungua rasmi Mkutano Mkuu wa 148 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) uliofanyika katika kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha CIGG, Geneva nchini Uswisi jana - Machi 24. (Picha na IPU).

GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendesha kwa ushirikiano wa msunguko - kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

